

124

MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

**MKATABA WA KUKODISHA GARI-FUSO KWA AJILI YA KUSAFIRISHA VIFAA VYA
UJENZI-VYOO NA SINK**

KWA AJILI YA UJENZI WA CHUO CHA VETA RUFJI

MKATABA NA: PA/24/2021/2022/TRA/RUF/DVTC-10

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe **8 mwezi 03 - 2022**

KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha **PWANI, S.L.P. 30345, KIBAHA, PWANI** ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

M/S PASCHAL & SONS TRANSPORT COMMUSION AGENT wa S. L. P.70981 DAR ES SALAAM. (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mzabuni wa usafirishaji vifaa ") kwa upande mwingine.

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya RUFJI;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya RUFJI;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Mzabuni wa usafirishaji vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kazi za ujenzi wa Chuo cha VETA Wilaya ya RUFJI ambayo ujenzi wake unaendelea;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

1. GHARAMA ZA USAFIRISHAJI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania **1,600,000/=** kwa kuasafirisha vifaa vya ujenzi kutoka Dar es Salaam mpaka eneo la ujezi Utete Rufiji kama inavyoonekana kwenye jedwari hapo chini kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama za usafirishaji vifaa vya ujenzi"

Gharama za kazi zitakazofanyika katika kila jengo ni kama ifuatavyo:

S/N	STAGE	BEI ILIYOKUBALIKA
1	GHARAMA ZITAKAZOTUMIKA KUSAFIRISHA VIFAA VYA VYOO NA SINK, BATH TRAY KUTOKA KIWANDA CHA KAMAKA- DAR ES SALAAM KWENDA ENEO LA UJENZI UTETE RUFJI	1,600,000
	JUMLA	1,600,000

2. MABADILIKO YA GHARAMA ZA USAFIRISHAJI (TRANSPORTATION SUM ADJUSTMENT)

Gharama za usafirishaji hazitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko yoyote yaliyofanywa na Mwajiri.

3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Malipo yatafanyika baada ya kazi kukamilika yaani Mzigo kufika eneo la ujenzi ukiwa salama na kwa idadi na kiwango kilichotakiwa.

4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI

(a) Mzabuni wa usafirishaji atakabidhi mzigo kwa wahusika wakuu waliopo eneo la ujenzi na kusainisha hati za mapokezi na nyaraka zingine muhimu kuonesha uhalali wa mapokezi ya mzigo husika.


(b) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Mzabuni wa usafirishaji kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo pasipo kuathiri pande zote.

5. WAJIBU WA MZABUNI WA USAFIRISHAJI

Mzabuni atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kusafirisha mzigo wa vifaa vya ujenzi kwa kadri alivyokubaliana katika mkataba sambamba na maelekezo ya Mwajiri.

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA
PWANI (PWANI RVTSC)

Jina: CLARA KUBODYA Saini: 


Wadhifa: KAIMU MCHU WA CHUO Tarehe: 08/03/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: LUKA C. MKINI Saini: ~~LUKA~~

Wadhifa: MKINI KAMATI YA
USENZI Tarehe: 08/03/2022

IMESAINIWA NA MZABUNI WA USAFIRISHAJI

Jina: PASCAL RANWA Mbele ya Saini: 
Wadhifa: DIRECTOR Tarehe: 8/03/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: JULIUS SONAS Saini: 

Wadhifa: DIRECTOR/ASSI Tarehe: 8/3/2022